Je, juhudi za Serikali zimesaidia vita dhidi ya rushwa?

Mtazamo wa watu kuhusu rushwa nchini Tanzania

1. Utangulizi

Miaka ya hivi karibuni, Tanzania imechukua hatua mbalimbali za kupambana na rushwa. Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 iliiongezea mamlaka taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). TAKUKURU imepanuka kwa kiasi kikubwa tangu kuanzishwa kwake, ikiwa ni pamoja na kuongezwa kwa bajeti, ujenzi wa makao makuu jijini Dar es Salaam, uanzishwaji wa ofisi za mikoa na wilaya na kuajiriwa kwa wafanyakazi zaidi[1]. Kama chombo kikuu cha Serikali cha kupambana na rushwa, kimeongoza katika uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa na Mikakati na Mipango Kazi (NACSAPs) katika ngazi ya kitaifa na ngazi za mitaa.

Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya 2010, Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 pamoja na sheria nyingine kadhaa zilizooneshwa kwenye tovuti[2] ya TAKUKURU zikiwa zimeandaliwa kuweka misingi imara wa kisheria ili kupambana na rushwa. Aidha, kwa msaada wa wafadhili, mageuzi kadhaa ya usimamizi wa fedha za umma (PFM) yamefanyika. Nchi yetu pia ni moja kati ya wanachama wa mipango mbalimbali ya kupambana na rushwa kama vile Mpango wa Uwazi Sekta ya ujenzi (COST), Mpango wa Kuendesha shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP) na Mpango wa Uwazi katika Sekta ya Madini Tanzania (TEITI).

---

[1] Tanzania Governance Review 2012: Transparency with Impunity?, Policy Forum [http://www.policyforum-tz.org/sites/default/files/TANZANIAGOVERNANCEREVIEW2012revised_0.pdf]

[2] PCCB http://www.pccb.go.tz/index.php/laws

Muhtasari huu umeandikwa na kuchapishwa na Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania. Wachangiaji ni Angela Ambroz, Youdi Schipper, Elvis Mushi, Risha Chande na Rakesh Rajani. Takwimu zilikusanywa na Ipsos Tanzania. Umetolewa mwezi Agosti 2014.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | barua pepe: uwazi@twaweza.org
www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Je, juhudi hizi zimeleta mabadiliko? Mwaka 2012, kulikuwa na idadi kubwa ya maafisa waandamizi wa Serikali waliosimamishwa au kufukuzwa kazi kutokana na tuhuma zilizohusiana na rushwa, na katika kipindi cha muongo mmoja uliopita kumekuwa na ongezeko kubwa la kuibuliwa kwa kashfa kubwa za rushwa. Ongezeka la mijadala mikali Bungeni, hasa mijadala inayogusa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)[3], pia imeweka shinikizo kwa Serikali kukabiliana na rushwa.

Hata hivyo, licha ya hatua hizi, Tanzania imeonesha kupunguza kwa kasi ya udhibiti wa rushwa katika miaka ya hivi karibuni na hii inaoneshwa katika Viashiria vya Utawala Duniani vinavyoandaliwa na Benki ya Dunia, udhibiti umeshuka kutoka 46 kati ya 100 mwaka 2007 hadi 22 mwaka 2012[4]. Vile vile Tanzania haijapiga hatua kwenye faharasa ya mitazamo kuhusu rushwa ya taasisi ya Transparency International, ikiwa tumeshuka kutoka alama 35 kati ya 100 mwaka 2012, hadi alama 33 mwaka 2013, na imeshika nafasi ya 111 kati ya nchi 177[5].

Aidha, kati ya mwaka 2008 na 2011 idadi ya tuhuma zilizopelekwa TAKUKURU na wananchi zilishuka kwa 22%, hii ikiashiria kushuka kwa imani ya wananchi kuhusu uwezo wa taasisi hiyo. Idadi ya kesi zilizokamilishwa na kupelekwa kwenye vyombo vya maamuzi na matukio ya hatua za kiutawala kuchukuliwa pia ulionekana kushuka. Kufukuzwa au kusimamishwa kwa maafisa wa Serikali hadi sasa hakujapelekea mtu kufungwa au kupewa adhabu yoyote.

Rushwa inaendelea kutawala vichwa vya habari na ajenda za mijadala na midahalo ya umma. Mwezi Mei mwaka 2014, gazeti la The Citizen liliripoti kuwa *'Kigogo mla rushwa hakabiliwi kwa bidii'.* Gazeti la The Guardian lilitoa habari ya faharasa ya mitazamo ya rushwa ya shirika la Transparency International kuwa: *'TAKUKURU, Idara ya Mahakama, Polisi walaumiwa kwa kushuka faharasa ya mtazamo wa rushwa,*[6] na gazeti linalomilikiwa na Serikali la The Daily News lilichapisha makala ya maoni iliyosomeka, *'Rushwa imezifanya Kenya na Tanzania kuwa mapacha walioungana*[7].

Lakini je, wananchi wana maoni gani? Pia wanakumbana na yapi?

Muhtasari huu unaripoti takwimu za hivi karibuni zenye uwakilishi wa kitaifa kuhusu maoni ya wananchi kuhusu rushwa nchini Tanzania. Takwimu zimetokana na awamu ya 19 ya Sauti za Wananchi; utafiti wa kwanza Afrika kwa njia ya simu mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa (www.twaweza.org/sauti). Takwimu hizi zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa wa Tanzania Bara. Simu zilipigwa kwa wahojiwa 1425 kati ya tarehe 9 mwezi na tarehe 25 Juni 2014.

Matokeo muhimu ni:

- Zaidi ya robo tatu ya Watanzania wanafikiri kuwa rushwa imekithiri sana leo kuliko ilivyokuwa miaka 10 iliyopita.

---

[3] Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi http://www.nao.go.tz

[4] Benki ya Dunia, Viashiria vya Rushwa Ulimwenguni mwaka 2012 [http://info.worldbank. org/governance/wgi/index.aspx#home]

[5] Transparency International, 2013 [http://www.transparency.org/research/cpi/overview]

[6] http://www.ippmedia.com/frontend/?l=67712

[7] http://dailynews.co.tz/index.php/columnists/columnists/31757-rushwa imezifanya -tanzania-na-kenya-kuwa mapacha walioungana

- Rushwa imeenea pande zote za jamii: wananchi zaidi ya 50% wanaiona rushwa ikiwa katika sekta zote ukiachilia mbali na sekta ya biashara na mashirika ya dini.
- Wananchi 9 kati ya 10 wanaona rushwa inayotolewa kwa polisi ni kitu cha 'kawaida sana', na polisi inatazamwa kama kitengo chenye rushwa zaidi katika jamii.
- 60% ya Watanzania waishio bara wameshawahi kuombwa rushwa na afisa wa polisi - 43% wakiwa wamelipa rushwa hiyo.
- Kashfa kubwa ya rushwa inayojulikana zaidi ni ile ya Richmond ya mwaka 2006.
- 93% ya Watanzania waishio bara hawajawahi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwenye mamlaka husika katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.
- Takriban nusu ya Watanzania waishio bara hawafikirii kabisa kama rushwa itaweza kupungua.

2. Mambo saba kuhusu rushwa nchini Tanzania

Jambo la 1: Rushwa ina sura nyingi

Rushwa inaweza kutokea katika sekta nyingi na ngazi mbali mbali – kutoka tukio dogo kabisa kwenye jamii hadi matukio makubwa kwenye ofisi ya Serikali, kwa kutoa mkataba wa kipekee kwa kampuni maalum wa ujenzi kwa kutarajia kitu kidogo. Katika awamu hii ya utafiti, tulibuni mazingira kadhaa na tukawauliza wananchi: Je, hii ni rushwa?

Kielelezo cha 1: Je, hii ni rushwa?
(Asilimia ya waliojibu Ndiyo)



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi – Awamu ya 19, Juni 2014.*

Kwa ujumla, wananchi wana hisia kali kuwa kupeana fedha za ziada au fedha isiyo rasmi kwa ajili ya huduma ni rushwa (Kielelezo cha 1). Karibu wananchi wote (95%) wanaamini kuwa kutoa fedha ili kupigiwa kura ni rushwa wakati chini ya mtu mmoja kati ya watatu (31%) wanaona zawadi wanayopewa walimu baada ya mtoto kupata mafanikio bora ni suala tatanishi.

Jambo la 2: Watanzania wengi wanafikiri rushwa inazidi kukithiri

Walipoulizwa kama wanafikiri kuwa rushwa kwa ujumla imekithiri sana leo kuliko ilivyokuwa miaka 10 iliyopita, Watanzania 78% wanafikiri hivyo (Kielelezo cha 2). Idadi ilikuwa sawa na rushwa ya vigogo - 78% (rushwa kubwa kubwa, kiwango cha juu cha rushwa) na, rushwa 'ndogo ndogo' - 76% (shughuli za kila siku zinazohusisha kutoa/kupokea hongo), walisema wananchi. (takwimu hazijaoneshwa).

Kielelezo cha 2: Rushwa ikoje sasa ukilinganisha na miaka 10 iliyopita?



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi – Awamu ya 19, Juni 2014.*

Shirika la Transparency International liligundua idadi sawa na takwimu hizi, kwenye utafiti wake wenye uwakilishi wa kitaifa wa mwaka 2013 ulioitwa Utafiti wa Kipimo cha Rushwa Ulimwenguni[8]: Wahojiwa wa Tanzania walipoulizwa kama wanafikiri rushwa ilikuwa imeongezeka au kupungua kipindi cha miaka miwili iliyopita (2011 hadi 2013), 69% waliamini kuwa rushwa ilikuwa imeongezeka. 17% tu ndio waliosema kwa maoni yao, rushwa ilikuwa imepungua.

Jambo la 3: Wananchi wanaona rushwa imeenea sana katika jamii, na pia polisi na wanasiasa ndio wanaopokea rushwa kwa wingi

Inashangaza kuwa rushwa inachukuliwa kama kitu cha kawaida sana na kwa kiasi fulani si kitu kipya karibia sekta zote. Wananchi 50% wanafikiri hivyo. Sekta pekee zilizo chini ya kiwango hiki zilikuwa ni mashirika ya kidini na sekta za biashara (Kielelezo cha 3).

Kwa kuangalia sekta moja moja, Watanzania walikuwa na mtazamo uliokaribia kufanana: 89% walisema kuwa rushwa kwa polisi ni kitu cha 'kawaida sana'. Wanasiasa walishika nafasi ya pili ambapo wananchi -85% waliona kuwa rushwa ni kitu cha kawaida sana kwenye siasa.

[8] Transparency International, 2013. [http://www.transparency.org/gcb2013]

Kwa huduma za kodi na ardhi, wananchi 80% waliiona rushwa kuwa ni kitu cha kawaida kwenye huduma za kodi, na wananchi 79% waliiona rushwa kuwa ni kitu cha kawaida kabisa au kiasi kwenye sekta ya ardhi. Rushwa imeenea katika sekta za utoaji huduma: wananchi 82% wanaiona rushwa ikiwa ni kitu cha kawaida kabisa kwenye huduma ya afya na wananchi 70% wanafikiri hivyo kwenye elimu. Iligundulika pia kuwa zaidi ya nusu (55%) ya wananchi waliiona rushwa kama kitu cha kawaida sana au kiasi kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs).

Kielelezo cha 3: Mitazamo kuhusu Rushwa (kwa kila sekta)



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi – Awamu ya 19, Juni 2014.*

Jambo la 4: Watanzania 60% (waliokutana na polisi) wameshawahi kuombwa rushwa na polisi, na 43% wamewahi kutoa rushwa

Tuliwauliza Watanzania kuhusu taratibu walizofuata mara ya mwisho walipotembelea ofisi ya Serikali au mtoa huduma katika sekta binafsi, kama vile kamati za maji za kijiji, Mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya dini, au shule za zilizo maeneo yao. Kisha tukawauliza kama waliombwa na/au kutoa rushwa.

Katika karibu kila sekta, idadi kubwa ya wananchi waliripoti kuwa walishawahi kuombwa rushwa (Kielelezo cha 4). Wananchi watatu kati ya watano (60%) waliombwa rushwa na polisi na mwananchi mmoja kati ya watatu (34%) aliombwa rushwa wakati alipokuwa akitafuta kazi.

Kutokana na hali hii, tuliwauliza; ni mara ngapi wao hutoa rushwa? Kwa mara nyingine tena polisi waliongoza kwa kupokea rushwa: Watanzania 43% walikiri kutoa rushwa kwa afisa wa polisi walipokutana naye mara ya mwisho (Kielelezo cha 4). Hii inajumuisha watu wote walioambiwa watoe rushwa (41%) na wale waliotoa wenyewe bila kuambiwa (2%).

Hali nyingine ya rushwa inayotendeka sana ni ile ya ‘kutoa kitu fulani’ kwa wafanyakazi wa afya. Hii inaweza kuwa kwa mfanyakazi wa kituo cha afya cha umma kilicho eneo hilo, au kwa mtu anayefanya kazi sekta binafsi. Hapa, Watanzania 15% waliripoti kutoa ‘kitu fulani’.

Hii ni karibu mara tatu zaidi ya idadi ya wananchi wanaolipa malipo yasiyo rasmi kwa polisi ikilinganishwa na malipo kwa wafanyakazi wa afya. Takwimu za utafiti kutoka sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) kwa ulinganifu, zinaonyesha kuwa kiwango chake kiko chini ila bado imebainika kuwa angalau mwananchi mmoja kati ya saba (13%) aliliripoti kuombwa rushwa.

Tukitumia utafiti wa Kipimo cha Rushwa Duniani wa 2013 uliofanywa na shirika la Transparency International, tunaweza kufanya ulinganisho wa juujuu kati ya Tanzania na wastani wa kimataifa kwenye suala la jinsi gani watu walitoa hongo au rushwa. Katika kesi hii, Watanzania walikuwa wanalipa hongo kwa maafisa wa polisi mara nyingi zaidi kuliko wastani wa kimataifa (nchini Tanzania watu 43% waliliripoti kutoa hongo kwa maafisa wa polisi ikilinganishwa na 34% ya wastani wa kidunia); walikuwa wanalipa mara chache kwenye masuala yanayohusiana na ardhi (10% nchini Tanzania dhidi ya 21% za kimataifa) na elimu (5% nchini Tanzania ikilinganishwa na 16% ya kimataifa) angalia (Kielelezo cha 4).

Kielelezo cha 4: Je, uliombwa kutoa rushwa? Ulitoa? (Kwa kila sekta)



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi – Awamu ya 19, Juni 2014.*

Jambo la 5: Watanzania wachache sana wanajua maelezo ya kashfa kubwa za rushwa

Tuliwauliza wahojiwa kuhusu kashfa za rushwa zilizoripotiwa kwenye vyombo vya habari (Kielelezo cha 5); kama walizijua kashfa hizo na wanaweza kuzitolea maelezo muhimu.

Kielelezo cha 5: Ufahamu wa kashfa za rushwa za hivi karibuni



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi – Awamu ya 19, Juni 2014.*

1. IPTL- Benki Kuu ya Tanzania, ikiwa imeizuia akaunti ya kampuni ya kufua umeme ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL) na ya Wizara ya Nishati na Madini, iliyotoa dola milioni 122 kutoka kwenye akaunti hiyo kwenda kampuni ya Pan African Power Solutions Tanzania[9]. Mashitaka yalifunguliwa kwenye mahakama nchini Uingereza mwezi Aprili 2014 na Benki ya Standard Chartered-Hong Kong kwa ajili ya kutolewa kwa fedha hizo[10].
2. David Jairo - Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini alituhumiwa mwaka 2011 kutoa rushwa kwa Wabunge ili kupitisha bajeti ya wizara yake.[11]
3. BAE Rada - Kampuni ya Uingereza, inayoitwa BAE Systems, ilitozwa faini na Serikali ya Uingereza mwaka 2010 kwa ajili ya kulipa rushwa ya dola milioni 12 ili kupata mkataba wa kuiuziaTanzania mfumo wa rada.[12]
4. EPA - Malipo ya Ulaghai ya fedha zipatazo dola milioni 116 yaliyotolewa na Benki Kuu kwenye akaunti za Malipo ya Madeni ya Nje ya Tanzania (EPA) mwaka 2005/2006[13].

[9] Lugongo, B. "CAG, Kamati ya Bunge kukutana kujadili suala la zaidi ya dola milioni 122 za IPTLl." The Citizen, 12 Machi 2014.
[10] "Vita ya mabilioni ya IPTL's yahamia mahakama ya ." The Citizen. 1 April 2014.
[11] "Tanzania: Kashafa ya Sh Bilioni 1 inaweza kugharamu ajira ya Katibu Mkuu." AllAfrica.com, 18 Julai 2011. [http://allafrica.com/stories/201107190568.html]
[12] Taylor, B. "Malipo ya BAE kwa Tanzania yanadhoofisha haki na uwajibikaji." The Guardian, 20 Machi 2012.
[13] "Bank of Tanzania (BoT) External Payments Arrears (EPA)." International Centre for Asset Recovery. [http://www.assetrecovery.org/kc/node/c3db0290-6a0e-11de-805d-551e161363cd.0;jsessionid=C410542627EC20B130EAC8803D03488A]

5. Richmond - Baada ya kutolewa zabuni ya kuzalisha nishati ya dharura kwa kampuni ya Richmond Development mwaka 2006, kupitia mchakato wa siri wa zabuni, ni wazi kuwa jenereta zenye kufanya kazi hazikutolewa licha ya malipo makubwa kulipwa kwa kampuni hiyo. Baada ya shinikizo kubwa kutoka kwa umma, Waziri Mkuu wa wakati huo alijiuzulu mwaka 2008[14].

Maelezo ya kashfa hizi (madai au kuthibitika) yametolewa kwa ufupia hapa chini. Kumbuka hizi zilikuwa kesi za rushwa kubwa kubwa za viongozi waandamizi Serikalini zilizo andikwa sana na vyombo vya habari na kujadiliwa kwa kina na umma. Twaweza kuuliza maswali haya haimaanishi kuwa tuna msimamo fulani kwenye suala hili:

Karibu 37% ya Watanzania hawajawahi kusikia chochote kuhusu kesi hizi (na 0.7% tu ndio wanaojua maelezo ya kesi zote). Kesi ambayo haikujulikana sana ni ile ya IPTL, wakati kesi iliyojulikana zaidi ni ile ya Richmond, ambayo pia ni moja ya kashfa kongwe tulizoulizia maelezo yake. (Hata hivyo, kumbuka kuwa, utafiti ulifanywa kabla ya kuibuliwa suala jingine la hivi karibuni kuhusu IPTL mwezi Julai 2014). Waliohojiwa kundi lililo kwenye mabano walikuwa na uwezo mkubwa wa kujua kuhusu kashfa hizi. Wananchi wenye elimu zaidi walikuwa pia na ufahamu mkubwa kuhusu kashfa hizi; ikiwa wananchi 9 kati ya 10 (86%) ambao wamemaliza kidato cha 4 dhidi ya wananchi 6 kati ya 10 (60%) ambao hawamaliza kidato cha nne.

Kielelezo cha 6: Ufahamu wa kashfa, kwa makundi ya watu
(Asilimia ya washiriki ambao wamewahi kusikia angalau kashfa moja)



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi – Awamu ya 19, Juni 2014.*

Ni dhahiri kuwa uelewa wa kashfa kubwa za rushwa upo chini, licha ya kutangazwa sana na vyombo vya habari na hoja za mijadala ya kisiasa. Ilibainika pia kuwa kuna tofauti katika upatikanaji wa taarifa kati ya wananchi matajiri pamoja na wale walioelimika zaidi. Kwa mfano, 84% ya Watanzania, kundi la matajiri wamewahi kusikia angalau kashfa moja,

[14] "Waziri Mkuu wa Tanzania kujiulu kutokana na rushwa." BBC, 7 Februari 2008. [http://news.bbc.co.uk/2/hi/africa/7232141.stm]

wakati 47% tu ya wananchi maskini zaidi ndio waliowahi kusikia angalau kashfa moja (Kielelezo cha 6). Idadi sawa na hiyo pia imejitokeza kwenye viwango vya elimu- Watanzania 86% waliomaliza kidato cha 4 ndio waliowahi kusikia angalau kashfa moja, wakati 49% ya wale ambao hawakuhitimu darasa la 7 walisikia angalau kashfa moja (takwimu hizi hazijaoneshwa).

Jambo la 6: Wananchi 51% wamekata tamaa kuhusu vita dhidi yarushwa nchini

Zaidi ya nusu ya Watanzania (51%) hawaamini kabisa kama rushwa inaweza kupunguzwa, na 34% wanafikiri kuwa inaweza kupunguzwa lakini kwa kiwango kidogo tu (Kielelezo cha 7). Hata hivyo, ukiangalia umuhimu wake kisiasa, kwa mfano kwenye uchaguzi ujao wa Serikali za mitaa na ule wa kitaifa: Watanzania walio wengi (70%, takwimu hizi hazijaoneshwa) hawaamini kuwa vyama vya upinzani vingefanya kazi nzuri zaidi ya kupambana na rushwa kama wangekuwa madarakani.

Kielelezo cha 7: Ni kwa kiasi gani unafikiri rushwa inaweza kupunguzwa nchini Tanzania



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi – Awamu ya 19, Juni 2014.*

Jambo la 7: Chini ya nusu ya Watanzania wanajua mahali pa kuripoti rushwa

Sehemu ya kukata tamaa kuhusu kutokomeza rushwa inaweza kuchangiwa na kukosa uelewa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali kushughulikia rushwa: Ni Mtanzania mmoja tu kati ya wanne anayefahamu Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu nchini Tanzania (NAOT). Vile vile ni mwananchi mmoja tu kati ya wananchi watano (20%) aliyejua ripoti za Ofisi ya Ukaguzi zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu (CAG), ni 4% tu ndio waliowahi kuziona ripoti hizo. Wahojiwa walipoelezwa matukio mbali mbali ya rushwa yaliyobainishwa kwenye ripoti ya CAG ya mwaka 2012/2013 , wananchi 75% walisema kuwa wanaamini mtu anapaswa kuwajibishwa kwa upotevu wa fedha za umma.

Zaidi ya hayo, chini ya nusu (44%) walijua sehemu ya kuripoti kitendo cha rushwa (na kati yao, 76% walifahamu kwa usahihi kuwa ni kwenye Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)) (Kielelezo cha 8). Licha ya kukumbwa na kusambaa kwa vitendo vya rushwa kulikosemwa na wananchi, idadi kubwa ya wananchi (93%) hawajawahi kuripoti tukio lolote la rushwa sehemu husika ndani ya kipindi cha miezi 12 iliyopita.

Kielelezo cha 8: Unafahamu mahali pa kuripoti vitendo vya rushwa? Na je, ni wapi?



Chanzo cha Takwimu: *Sauti za Wananchi – Awamu ya 19, Juni 2014.*

3. Hitimisho

Muhtasari huu unatoa matokeo ya kushangaza kuhusu viwango vya rushwa kwenye maisha ya kila siku ya kila Mtanzania. Wananchi wanakiri wazi kuwa kupeana fedha zisizo rasmi ni rushwa. Katika sekta zote (usalama, siasa, kodi, ardhi, afya, elimu, maji, Serikali za mitaa, na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs)) ukiachilia mbali biashara na mashirika ya dini, wananchi zaidi ya 50% wanaona rushwa kuwa ni kitu cha kawaida sana au kwa kiasi fulani cha kawaida. Kwa ujumla, wananchi hutoa rushwa wakiwa kwenye hali tete, kwa mfano wanapokutana polisi au kuhitaji huduma za afya. Kiidadi, wahojiwa watatu kati ya watano wanaripoti kuwa, rushwa iliombwa walipokutana na polisi mara ya mwisho. Hii ni karibu mara mbili ya uombwaji rushwa unaoshika nafasi ya pili, wakati wananchi wakiwa wanatafuta ajira.

Rushwa inatazamwa kama kitu cha kawaida kabisa au cha kawaida kiasi kwenye huduma zote za Serikali (na wahojiwa zaidi ya 65%), ukiondoa na sekta ya maji (labda kwa sababu huduma za maji kwenye maeneo ya vijijini kwa kiasi kikubwa haziendeshwi na Serikali). Wakati sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali imepewa nafasi ya chini kwenye rushwa ikilinganishwa na ofisi nyingi za Serikali, mashirika hayo yasiyo ya kiserikali yanaonekana kuwa na rushwa zaidi kuliko sekta ya biashara. Ili kulinda na kurejesha uaminifu wake, jumuiya ya kashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) wanaweza kuaanda kanuni za maadili za wazi na mbinu madhubuti za kudhibiti vitendo vyao wenyewe.

Tofauti na uzoefu mkubwa wa rushwa unaofanyika kila siku, wananchi kwa kiasi kikubwa hawajui kashfa kubwa za rushwa za hivi karibuni, licha ya kuandikwa sana kwenye vyombo vya habari na mijadala ya kina bungeni na kwenye jamii. Karibu nusu ya Watanzania (44%) walikuwa hawajawahi kusikia kuhusu kashfa ya Richmond, na wachache zaidi walikuwa wanafahamu kashfa nyingine kubwa. Matokeo haya yanaibua maswali ya kuvutia juu ya umuhimu na uzoefu wa rushwa katika maisha ya watu wengi. Kwanza, uelewa mdogo wa rushwa na shauku ndogo ya kufuatilia kashfa kubwa za rushwa unaonesha kuvunjika kwa muafaka wa kijamii na kisiasa (social and political compact) kati ya Serikali na wananchi. Rasilimali zinazotumiwa vibaya ni mali za Watanzania wote, na watumishi wa umma wanaoshiriki kufuja fedha za umma wameajiriwa na Watanzania. Kuandikwa kwa kashfa kwenye vyombo vya habari kunalenga kujenga ufahamu na umma kushinikiza uwajibikaji. Lakini wahojiwa wengi hawakuona uhusiano kati ya rushwa kubwa na hali zao za maisha.

Ukweli ni kwamba jitihada za kupunguza rushwa hazijazaa matunda na pia ina maana kuwa hakuna mwitikio wa kutosha kutoka chama kilicho madarakani. Vile vile udhaifu upo kwa upande wa vyama vya kiraia kuhamasisha na kuelekeza hatua za kuchukua kwa pamoja[15]. Wakati huo huo, zaidi ya theluthi mbili ya Watanzania hawafikiri kama vyama vya upinzani vingefanya chochote cha tofauti kupunguza rushwa, licha ya kuizungumzia rushwa mara kwa mara. Kwa ujumla, wananchi wengi waliohojiwa wamekata tamaa kuwa hakuna mtu yeyote anayeweza kulishughulikia swala la rushwa ipasavyo. Hali hii ikiangaliwa kwa undani, inaonekana kuwa kuna tatizo kubwa la imani ya wananchi juu ya taasisi zote ndani ya jamii.

Wakati huo huo, matokeo yanaonesha kuwa wakati wanasiasa, vyombo vya habari, NGOs, wafadhili na wananchi wenye elimu bora wanajikita zaidi kwenye kashfa kubwa, Watanzania wengi wanaonekana kuangalia zaidi aina ya rushwa ambayo inawagusa moja kwa moja na kuathiri maisha yao ya kila siku. Wakati hitaji la kuelezea kwa kina jinsi rushwa kubwa inavyoathiri wananchi wa kawaida liko wazi dhahiri, tabaka la wasomi na watu wenye nafasi katika jamii wanaweza kuwa wanafanya makosa kuichukulia rushwa ya kila siku kama ‘ndogo’; kwa kulazimika kulipa kitu mara kwa mara kwa polisi au wahudumu wa afya au maafisa ardhi ni mzigo mkubwa kwa maskini. Wakati rushwa kubwa hutangazwa sana kwa sababu inahusisha kiasi kubwa cha fedha na watu maarufu, wale ambao wanataka kuwakilisha vyema maslahi ya watu na kuendeleza ustawi wa wananchi, watafanya vyema kuweka umakini mkubwa kwenye rushwa ya kila siku, na jinsi inavyoweza kutatuliwa. Katika suala hilo, ni ukweli kuwa rushwa mara nyingi zaidi huombwa kuliko kutolewa, kuna uwezekano mkubwa wa kukabiliana na tatizo hili. Kwanza, watoa huduma za Serikali wanaweza kutafuta njia za wananchi kutoa taarifa kuhusu kuombwa rushwa- tunaweza kujifunza kutokana na uzoefu wa taasisi za nchi mbalimbali kama vile IPaidaBribe.com nchini India. Hata hivyo, ili hili liweze kuwa na tija hatua kadhaa za kujenga imani kwa wananchi zitahitaji kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na njia za kutoa taarifa kwa watumiaji kama; uchapishaji wa haraka wa ripoti katika namna ambayo inaweza kuonekana na kusikika na watu wengi (kwa mfano, kupitia radio); hatua za haraka za Serikali katika kukabiliana na tatizo, na kuonesha bidii na umakini; na ulinzi wa kutosha wa usiri wa mchakato wa kutoa taarifa.

[15] Pia ni mashitaka makubwa ya wafadhili ambao wametumia mabilioni ya shilingi ya kupunguza rushwa kwenye program/mi-pango ya serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali na wafanyakazi wao.

Pili, kwa vile sio wote wanaoombwa rushwa hutoa, itakuwa na manufaa kuwatathmini, kutunza kumbukumbu zao na kuandika wasifu wa wale wote waliokataa kutoa rushwa. Kwa kifupi, kama mamlaka zina nia ya kuhakikisha Serikali yenye uwazi, wanahitaji kuanzisha utaratibu madhubuti na wenye tija wa kuwa na sehemu ya wananchi kukimbilia kupata msaada pindi wanapoombwa rushwa, na wananchi kufahamishwa sehemu hiyo.

Mapendekezo haya siyo mapendekezo pekee bora, lakini yanalenga kuonesha njia za kufikiria kuhusu kukabiliana na rushwa. Matokeo haya ya utafiti yanaonesha kuwa licha ya jitihada za kuboresha utawala na ahadi za mara kwa mara za uwazi Serikalini, ukweli ni mambo matatu yanatawala: rushwa imeenea kote kwenye maisha ya kila siku ya wananchi; hali ya rushwa inazidi kuwa mbaya; na wananchi hawaamini kuwa Serikali au upinzani wanaweza au wataweza kupunguza rushwa. Nchi yetu kuendelea na hali hii si busara, na pia kuendelea kujidanganya kuwa tunapiga hatua nzuri kunaweza kuleta anguko letu. Wananchi wakikosa imani kwa taasisi zao na viongozi wao, kunaweza kusababisha kuvunjika kwa amani ndani ya nchi.